**HOTUBA YA UFUNGUZI YA MWENYEKITI WA BARAZA LA WAFANYAKAZI LA MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA (TMA) DKT.AGNES KIJAZI TAREHE 30/03/2016 KATIKA UKUMBI WA UDBS, CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM.**

**Mgeni Rasmi Mwakilishi wa mwenyekiti wa Bodi ya Shauri ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Engineer James Ngeleja.**

**Wakurugenzi na Mameneja wa Mamlaka ya Hali ya Hewa,**

**Mwenyekiti wa Tughe Mamlaka ya Hali ya Hewa,**

**Viongozi wa Matawi ya TUGHE ya Mamlaka,**

**Wajumbe wa Baraza,**

**Wanahabari,**

**Wageni waalikwa,**

**Mabibi na Mabwana.**

Awali ya yote nitumie nafasi hii kwa niaba ya wajumbe wa baraza na wafanyakazi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania kukushukuru mheshimiwa mgeni rasmi kwa kukubali kuja kutufungulia kikao hiki cha Baraza la wafanyakazi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania. Tunatambua majukumu mengi uliyonayo, lakini bado umeona ni muhimu kufika kulifungua baraza hili rasmi. **Tunakushukuru sana.**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Mamlaka ya Hali ya Hewa kwa kutambua na kukidhi matakwa ya kisheria ya kuwepo Baraza la wafanyakazi katika sehemu za kazi, imekuwa ikifanya vikao vyake vya Baraza kila mwaka. Baraza hili limewashirikisha viongozi wa Mamlaka na wawakilishi wa wafanyakazi kutoka katika vituo

vya hali ya hewa vilivyoko katika maeneo mbali mbali hapa nchini kwa kuzingatia muundo wa mkataba wa Baraza.

Katika kikao hiki cha baraza la wafanyakazi, wajumbe watajadili bajeti ya Mamlaka kwa mwaka wa fedha 2016/17, kupitia utekelezaji wa masuala yote yaliyojadiliwa na kuwekewa maazimio katika baraza lililopita, kuangalia mafanikio na pia kuweka vipaumbele kwa mwaka wa fedha 2016/17. Pia katika kikao hiki wajumbe wataendelea kukumbushwa majukumu na wajibu wao wakiwa kama watumishi wa umma. Pamoja na hayo wajumbe pia watapata nafasi ya kusikiliza mada mbali mbali kutoka kwa wataalam waliobobea katika masuala ya utumishi wa umma.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Mamlaka ya Hali ya Hewa imeendelea kutimiza majukumu yake katika kuchangia maendeleo ya Taifa. Katika hili tumeendelea kuongeza ubora na usahihi wa utabiri wa hali ya hewa wa kila siku, siku kumi, mwezi na msimu, kwa matumizi ya sekta mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kilimo, usafirishaji, ujenzi, na sekta zote za uchumi na kijamii kwa ujumla.

Katika mapitio ya utabiri wetu kwa msimu uliopita yaani Oktoba mpaka Desemba 2015, usahihi wa utabiri wetu umefikia kiwango cha asilimia **85.8,** haya ni mafanikio makubwa. Hata hivyo mafanikio haya yanachangiwa kwa kiasi kikubwa na serikali kwa kutambua umuhimu wa sekta ya hali ya hewa katika maendeleo ya nchi na hivyo kuiwezesha Mamlaka kupata vifaa vya kisasa pamoja na wataalam wake kupata mafunzo mbali

mbali ndani na nje ya nchi. Vifaa hivyo ni pamoja na Rada za hali ya hewa, mitambo ya hali ya hewa inayojiendesha yenyewe, mitambo ya uchambuzi na mitambo ya mawasiliano. Aidha, Ushirikiano na nchi zilizoendelea katika masuala ya hali ya hewa umechangia pia katika kuboresha huduma za hali ya hewa hapa nchini.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi, wajumbe wa baraza mabibi na mabwana,**

Ninayo furaha kuwajulisha watanzania kwamba huduma za hali ya hewa zinazotolewa hapa nchini zimeendelea kuboreshwa na kukidhi viwango vya kimataifa. Mamlaka ya Hali ya Hewa imeendelea kushikilia cheti cha ubora kinachotambuliwa na shirika la viwango nchini katika utoaji wa huduma za hali ya hewa katika usafiri wa anga, hii inatokana na ukaguzi uliyofanywa na taasisi ya kimataifa ya Certech iliyoka Canada kwa miaka 5

mfululizo ambapo ukaguzi umekuwa ukifanyika mara moja kila mwaka kuanzia mwaka 2010, ambapo kwa vipindi vyote wakaguzi hao wamesifu kuongezeka kwa ubora wa huduma zinazotolewa. Nichukue nafasi hii kuwapongeza wafanyakazi wa mamlaka ya hali ya hewa kwa kazi nzuri wanayofanya.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Wafanyakazi wa Mamlaka ya hali ya hewa kama walivyo watumishi wengine katika utumishi wa umma tumejipanga kuhakikisha tunafanya kazi zetu kwa weledi, uadilifu, juhudi na maarifa katika kutimiza wajibu wetu ili kuchangia katika kutekeleza malengo ya serikali yenye kusudi ya kuleta maendeleo na kuondoa umaskini hapa nchini. Tunafahamu wazi kwamba majanga yanayosababishwa na hali mbaya ya hewa yamekuwa yakirudisha nyuma maendeleo. Hivyo

tutaendelea kuboresha huduma za hali ya hewa na kuandaa utabiri mahususi kwaajili ya kutumika katika sekta mbali mbali za maendeleo. Na pia tutaendelea kutoa tahadhari za hali mbaya ya hewa kwa wakati. Ombi letu kwa umma wa watanzania muendelee kufuatilia taarifa za hali ya hewa na kuzitumia katika shughuli zenu za kila siku. Napenda kuvishukuru vyombo vyote vya habari hapa nchini kwa kushirikiana na TMA kuhakikisha taarifa za hali ya hewa zinawafikia walengwa kwa wakati. Tuna njia nyingi za mawasiliano zinazotuwezesha kufikisha taarifa za hali ya hewa kwa walengwa lakini vyombo vya habari ndivyo vinavyochukua nafasi ya kwanza kwani wananchi wengi wanasikiliza, wanatazama na kusoma habari kupitia vyombo hivyo.

**Mheshimiwa mgeni rasmi**

Kwa mara nyingine tena, ninapomalizia taarifa yangu hii fupi narudia kukushukuru kwa kujumuika nasi hapa leo. Napenda kukuhakikishia kuwa yale yote utakayo elekeza tutayafanyia kazi kwa nguvu, maarifa na weledi mkubwa. Sisi watumishi wa TMA tunatekeleza kauli mbiu ya HAPA KAZI TU kwa vitendo kwani tunafanya kazi saa 24 siku saba katika wiki bila kujali mchana au usiku, jua kali au mvua, joto au baridi, upepo mkali au hali ya utulivu taarifa za hali ya hewa zinasomwa kila baada ya nusu saa watumishi wa TMA hutoka nje ya ofisi kusoma taarifa hizo za hali ya hewa. Hivyo lolote utakaloagiza lililosehemu ya majukumu yetu litatekelezwa kwa wakati. Napenda pia kuishukuru kamati ya maandalizi ambao wamefanya kazi kubwa ya kuandaa baraza hili, Asanteni sana.

Kwa heshima sasa, Mheshimiwa mgeni rasmi, naomba nikukaribishe ili uzungumze na wajumbe wa Baraza na kisha utufungulie Baraza hili la wafanyakazi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania. Mheshimiwa mwakilishi wa mwenyekiti wa Bodi, Karibu.